# Kanuni za Ubuntu katika Methali za Kiswahili

*Lina Akaka*
*Chuo Kikuu cha Daystar*

**Ikisiri**

**Makala haya yalichanganua kanuni za ubuntu zinazojitokeza katika methali za Kiswahili. Kanuni za ubuntu zinadhihirika katika methali sio tu za Kiswahili bali za jamii mbalimbali za Kiafrika. Waafrika walitumia vipera mbalimbali vya fasihi simulizi kuelimisha na kuadilisha wanajamii (Akaka na Wandera-Simwa, 2024). Umoja wa kijamii pamoja na maadili mengine yanayokuza na kuhimiza uhusiano mwema baina ya Waafrika unadhihirika katika fasihi simulizi zao zikiwemo methali. Maadili ya kimaisha yanayosisitiza umoja na thamani nyinginezo miongoni mwa jamii za Kiafrika zimefumbatwa katika methali zao. Maana ya dhana ubuntu inatokana na mojawapo ya methali za jamii za Kiafrika. Ubuntu kama falsafa ilianza kutumiwa katika maandishi tangu mwaka wa 1846 lakini ufafanuzi wa dhana hii unatokana na methali ya Kingun*i umuntu ngumuntu ngabantu* (Gade, 2011). Mtafiti aliteua kimaksudi kamusi za methali za Wamitila (2001), King'ei na Ndalu (1989) na Omusikoyo (2021) ili kuchanganua kanuni za ubuntu zilizomo katika baadhi ya methali. Methali zilizo na kanuni za ubuntu ziliteuliwa kimakusudi. Kanuni za ubuntu zilizomo zikatambuliwa na kujadiliwa vile zinavyojitokeza katika methali za Kiswahili. Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi kwa mujibu wa Fairclough (1992) iliongoza utafiti huu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa methali za Kiswahili zimesheheni kanuni za ubuntu zinazozikumbusha jamii za Kiafrika kushirikiana, kupendana na kujaliana.**

**Maneno Muhimu:** *Ubuntu, Kiafrika, Methali, Utamaduni*

**Utangulizi**

Mila na utamaduni wa jamii za Kiafrika umefumbatwa katika simulizi zao zikiwemo methali (Akaka na Wandera-Simwa, 2024). Maitaria (2021) anaunga mkono wazo hilo anaposema kuwa methali hutokana na utamaduni wa watu na hutumika katika kuibulia na kuelekezea busara ya wenyeji. Methali za Kiswahili zimeibuliwa kutoka jamii mbalimbali za Waswahili kote katika ukanda wa Afrika Mashariki na yaliyomo yanatokana na matarajio yao kuhusu jinsi wanavyohusiana wenyewe kwa wenyewe. Utamaduni wa Mwafrika unasisitiza kutegemeana, kwamba mtu hawezi kuishi kama kisiwa. Wazo kama hilo linafafanua zaidi kwa nini methali za Kiswahili zimesheheni kanuni za ubuntu zinazokuza maadili ya haki, uwajibikaji, usawa, umoja, uhusiano, upendo, heshima, utu, usaidianaji, ujamaa, utegemeanaji na kujaliana miongoni mwa wanajamii (Mayaka na Truell, 2021).

Mayaka na Truell wanaendelea kueleza kwamba ubuntu hulenga ujumlishwaji wa kila mtu ndani ya jamii, wajibu wao kwa wengine na ustawi wa mazingira ili kuhakikisha ushindi kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ubuntu ni falsafa ya Kiafrika inayosisitiza ujamaa, kujaliana na kutegemeana. Ubuntu ni falsafa ambayo imekuwepo kwa muda mrefu na hujitokeza katika mtindo wa maisha ya Waafrika. Kimsingi maisha ya jamii za Kiafrika yaliongozwa na kanuni za falsafa ya ubuntu. Komparic (2015) na Cilliers (2008) wanashadidia wazo hilo wanapoeleza ubuntu ni mfumo wa maadili ya Kiafrika ambao umekuwa na athari kubwa katika eneo kubwa la kijiografia kwa kipindi cha muda mrefu, kusini mwa Sahara. Wanaendelea kuhoji kuwa falsafa hii ina asili yake katika kipindi cha kabla ya ukoloni na ni mfumo wa kawaida wa kimaadili miongoni mwa Waafrika hususan Waafrika wa Afrika Kusini. Metz (2009) anaongeza kuwa ubuntu hujumlisha maadili, mkondo wa mawazo na kaida za maisha zinazopendelewa miongoni mwa Waafrika. Falsafa ya ubuntu ina kanuni nyingi lakini makala haya yalizichunguza tu baadhi yake katika methali za Kiswahili. Kanuni hizi hujitokeza katika simulizi za kimapokeo za Waafrika. Simulizi hizo zikiwemo methali huakisi kaida, thamani na maadili ya Waafrika na zilitumiwa kuadilisha jamii kabla ya kuja kwa wakoloni. Methali ni mojawapo ya nyenzo kuu zilizotumika kupitisha maadili ya jamii kutoka kizazi hadi kingine hivyo zimesheheni kanuni za falsafa ya ubuntu.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi kwa mujibu wa Fairclough (1992). Fairclough aliiasisi nadharia hii na ikaendelezwa na Gunther Kress, Teun van Djik, Theo van Leeuwen, Ruth Wodak na wengineo. Fairclough aliandika vitabu vya kisemina *Language and Power* cha 1989 na *Discourse and Social Change* cha 1992 ambavyo viliweka msingi wa nadharia hii. Katika kuiendeleza nadharia hii, Van Dijk (2008) ambaye alieleza vile diskosi zimekitwa katika utamaduni na kutoa mchango kwenye miundo pana ya utamaduni na jamii. Kress (2010) alichangia kwenye nadharia hii pia. Alieleza vile miktadha ya kiutamaduni na kijamii inavyoumba ufasiri na uelewa wa ishara na vile njia mbalimbali za mawasiliano zinavyofanya kazi pamoja ndani ya miktadha hii ili kuzalisha maana. Van Leeuwen (2008) kama Kress (2010) alisisitiza umuhimu wa muktadha katika kuelewa diskosi. Alihoji kuwa diskosi zimekitwa ndani ya miktadha ya kiutamaduni, kijamii na kihistoria ambayo huumba na kuumbwa kwa njia ambazo maana inazalishwa na kufasiriwa. Wodak (1989) alitoa mchango mkubwa kwenye nadharia hii alipoanzisha mkabala wa kihistoria wa diskosi ndani ya nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi. Mkabala huo ulijenga msingi ambamo machapisho yake yaliyofuatia yalijengeka.

Kimsingi, Fairclough alianza kutoa wazo la diskosi kama shughuli ya kiutamaduni katika miaka ya thelathini baada ya chapisho lake la awali la kazi za kimsingi kuhusu uchanganuzi hakiki wa diskosi. Hata hivyo, wazo la diskosi kama shughuli ya kijamii lilianzishwa katika *Language and Power* (1989) na kuendelezwa zaidi katika *Discourse and Social Change* (1992). Kazi zilizofuatia za Fairclough zilieleza kwa upana kuhusu mikabala ya kiutamaduni ya diskosi. Kwa misingi hii nadharia ya Fairclough (1992) ilitumiwa kuongoza utafiti huu. Fairclough anasisitiza kuwa diskosi ni sehemu muhimu ya shughuli za kijamii na kiutamaduni. Anachunguza vile diskosi zinavyoumba na kuumbwa na michakato ya kiutamaduni, kaida na maadili. Fairclough (1992) anajumuisha vipengele vya kiutamaduni katika uchanganuzi wa diskosi akizingatia vile shughuli za lugha zinavyochangia katika uzalishaji na mabadiliko ya kiutamaduni. Anahoji kuwa diskosi hufanya kazi na kujenga mifumo ya maarifa na imani hivyo kuathiri shughuli za kiutamaduni. Lugha sio tu njia ya mawasiliano lakini ni shughuli ya kijamii ambayo imekitwa ndani ya michakato ya kiutamaduni na kiitikadi (Fairclough, 1992).

Kulingana na Fairclough (1992), nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi hujumuika na utamaduni ili kuchunguza vile diskosi zinavyoakisi na kuumba shughuli za kiutamaduni, kaida na uhusiano wa kimamlaka. Anaeleza kuwa diskosi ni aina ya shughuli ya kijamii ambayo imejikita katika miktadha maalum ya kiutamaduni na kihistoria. Hivyo basi diskosi huathiri na kuathiriwa na kaida pamoja na maadili ya jamii. Shughuli za kiutamaduni huonekana kujengwa, kuendelezwa na kubadilishwa kupitia kwa diskosi. Kwa misingi ya mawazo ya Fairclough (1992), mtafiti alichanganua vipengele vya lugha katika methali lengwa za Kiswahili kwa kutambua maneno yanayorejelea kanuni za ubuntu. Tamathali za usemi kama vile tashbihi na sitiari zilizotumiwa kupitisha maadili ya kijamii zilichunguzwa, miktadha zinamotumiwa katika mazungumzo ya kila siku pia ilichunguzwa kando na vile methali hizo zinavyotumiwa kuimarisha kaida za jamii na maadili ya kiutamaduni.

**Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ni wa kimaktaba. Mtafiti alipitia makala, vitabu na majarida maktabani pia mtandaoni ili kurejelea waliyoyasema wataalamu waliotangulia kuhusu kanuni ya ubuntu, nadharia ya Fairclough (1992) pia methali kwa jumla. Kundi lengwa la utafiti ni methali na sampuli lengwa ni methali za Kiswahili zilizo na kanuni za ubuntu. Mtafiti aliteua methali za Kiswahili kuzitafiti kwa sababu Kiswahili ndio lugha inayozungumzwa na idadi kubwa ya watu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati hivyo makala haya yatakuwa ya manufaa kwa idadi kubwa ya wasomi wa Kiswahili. Mtafiti aliteua kimaksudi diwani tatu kwa shughuli za utafiti. Methali zilizoteuliwa zilitolewa katika kamusi za King'ei na Ndalu (1989), Wamitila (2001) na Dira ya Methali, Omusikoyo (2021). Vifaa vya ukusanyaji data vilivyotumika katika utafiti ni kalamu, daftari, kipakatalishi na kamusi teule za methali. Mtafiti alichanganua data ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia ya Fairclough (1992). Kamusi tatu teule za methali zilipitiwa kwa umakinifu huku mtafiti akiteua kimaksudi methali zilizobeba kanuni za ubuntu ili kuzitafiti. Methali lengwa zilinakiliwa katika daftari na mtafiti akaziainisha na kuzifafanua chini ya mada ndogondogo za kanuni za ubuntu. Miktadha zinamotumiwa

ilifafanuliwa, kanuni za ubuntu zilizomo zikaelezwa kwa kuzifungamanisha na methali pamoja na muktadha zinamotumiwa katika maisha ya kila siku. Methali zenye kaida sawia ya ubuntu zilitumiwa ili kukamilishana na kujenga fasiri.

**Kanuni za Ubuntu**

Kanuni za ubuntu zimefumbata maadili na imani zinazosisitiza utegemeanaji, umoja wa kijamii na heshima ya binadamu. Eze (2010) amefasiri kanuni hizo akisisitiza uunganishwaji na vipengele vya kiuhusiano vya kuwepo kwa binadamu. Kama vile Eze, Metz (2007), anasema falsafa ya ubuntu ni nadharia ya kipekee ya kimaadili iliyokitwa katika falsafa za kiutamaduni za Kiafrika. Anaitofautisha na nadharia za Kimagharibi zinazochukulia kuwa kitendo kinacholeta furaha kwa watu wengi ni kanuni ya mwongozo wa maadili. Metz (2007) aliilinganisha pia na nadharia ya kimaadili ya Immanuel Kant ijulikanayo kama ukani. Nadharia hiyo ina mihimili mikuu mitano lakini Wood (2008) anafafanua mmojawapo akisema nadharia hiyo ililenga dhana za uwajibikaji, sheria ya maadili na kanuni inayotoa njia ya kutathmini iwapo kitendo kinaruhusiwa kimaadili au la. Tofauti na nadharia za maadili za Kimagharibi, Eze (2010) anafafanua kanuni kadha wa kadha za ubuntu zikiwemo utegemeanaji na ujamaa, heshima ya binadamu, huruma, umoja, ukarimu, haki na usawa, mshikamano wa kijamii, usaidianaji, msamaha na heshima kwa mazingira. Utafiti huu ulichanganua kanuni hizo katika methali za Kiswahili kwenye sehemu ifuatayo.

**Maadili ya Kiafrika na Ubuntu**

Ubuntu ni falsafa ya maadili ya Kiarika, (Metz 2007). Ni dhana ya Kiafrika inayorejelea utu baina ya watu katika jamii (Nyaumwe na Mkabela, 2007). Dhana ya ubuntu inapatikana katika tamaduni nyingi za Kiafrika ingawa inatofautiana tu kwa jina inayopewa katika jamii mbalimbali (Mugumbate & Chereni, 2019). Dhana ubuntu ina asili yake katika simulizi za wabantu wa Kinguni. Ingawa istilahi ubuntu ina uasili wake katika simulizi za Afrika Kusini, West (2013) anasema maana iliyomo imo katika tamaduni nyingine nyingi barani Afrika. Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa ubuntu ni utanzu wa falsafa ambao unaweza kurejelewa kama maadili ya Kiafrika (Hailey 2008, Metz 2007, Binsbergen, 2001). Mtindo wa maisha ya Waafrika uliongozwa na kanuni za ubuntu, Mbendera (2020). Mbendera anaendelea kueleza kuwa wakati wa kipindi cha utawala wa wakoloni, Waafrika walipitia wakati mgumu sana kiasi kwamba mfumo wao wa maadili ulivurugika na mtindo wao wa maisha pia.

Kabla ya majilio ya wakoloni, mfumo wa kiutamaduni wa maadili ya Waafrika ulilindwa na wazee pamoja na miiko (Mbendera, 2020). Anaendelea kufafanua wazee waliadhibu wanajamii waliokiuka maadili yaliyokubalika huku mila zikidhibiti namna watu walivyohusiana. Mila nyingi za jamii mbalimbali zilifumbatwa katika fasihi simulizi yao. Mila hizo zilifumbatwa katika ngano, mashairi, nyimbo, methali na simulizi nyinginezo. Methali za jamii mbalimbali zilifumbata mila hizo pia, zikiwemo za Kiswahili. Waafrika walitumia simulizi hizo katika mfumo wao wa elimu ya kiutamaduni. Walizitumia kuelimisha, kuadilisha na kushauri wanajamii. Simulizi zao nyingi zilijikita katika maadili yaliyotarajiwa kuwaelekeza wanajamii kwenye utu hivyo kuhusiana vyema kama anavyosema Maitaria (2021) kuwa methali zilitekeleza dhima ya uashiriaji, uelezaji na uelekezaji kuhusu maisha.

Methali hizo zinasheheni kanuni za falsafa ya ubuntu ambayo husisitiza umuhimu wa kutambua heshima na thamani ya kila mtu. Isitoshe husistiza pia kukuza umoja miongoni mwa wanajamii na kukumbatia uwajibikaji wa pamoja kwa ajili ya ustawi wa jamii kwa jumla, (Venter, 2004). Falsafa ya ubuntu inatawaliwa na kanuni zinazoongoza maadili ya watu binafsi pamoja na jamii licha ya kuumba uhusiano baina ya watu, kaida za jamii na uelekezaji wa tabia. Baadhi ya kanuni hizo ni kuunganika na kutegemeana, heshima ya binadamu, huruma, ujamaa na umoja, utulivu na amani, ukarimu na kufaana, haki na usawa, heshima kwa mazingira. Wana-nadharia mbalimbali wa nadharia ya maadili ya Waafrika wameeleza kanuni za ubuntu kwa njia tofautitofauti lakini zinazohusiana, (Ewuoso na Hall, 2019). Utafiti huu utafafanua kila kanuni ya falsafa ya ubuntu katika sehemu inayofuatia.

***Utu***

Utu ni kanuni mojawapo ya ubuntu inayosisitiza ubinadamu. Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21 (2019), utu ni hali ya kuwa na tabia nzuri ya kiutu; ubinadamu, kinyume cha unyama. Methali maarufu inayokuza kanuni hii ni *mtu ni utu.* Kinyume cha utu ni unyama, mtu asiyekuwa na utu basi

ana unyama na ana uwezo wa kuwatenda wengine kinyama. Methali hii inasisitizia watu kuwathamini binadamu wenzao. Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi kwa mujibu wa Fairclough (1992) inatumika kueleza vile methali ya *mtu ni utu* inavyoakisi uhusiano wa kimamlaka na mtagusano wa wanajamii. Methali hii kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi inaendeleza mabadiliko ya kijamii au uthabiti. Methali hii inakuza sifa ya utu kwa kila mtu kwa kuhimiza mielekeo na tabia ambazo zinaendeleza mshikamano wa kijamii na haki. *Mtu ni utu* ni methali inayowapa watu waliotengwa hisia za kuthaminiwa mbali na kupinga kaida zinazokandamiza. Katika muktadha ambamo mtu hujiona bora kuliko wengine na kuwadharau pengine kwa misingi ya uwezo wa kiuchumi au mamlaka aliyo nayo dhidi yao, huweza kupigiwa methali hizi.

Kuna methali nyingi za Kiswahili zinazokuza maadili ya utu ambayo pia ni kanuni ya falsafa ya ubuntu. Methali hizo huelekea kulenga watu waliofanikiwa kimaisha na kuwaonya kuwa wasiwadharau wasi navyo. Kwa mfano methali mpanda ngazi hushuka kama inavyoelezwa katika Wamitila (2001) anatoa maelezo ya methali *mpanda ngazi hushuka* akisema methali hii hutumiwa kumzindua mtu aliyepata mali, neema au madaraka kisha akawa anajitapa na kuwadharau wenzake. Anapaswa kujua kuwa haifai kuvimba kichwa kwani inawezekana siku moja akaishiwa na mali hiyo na kubakia kama wenzake anaowadharau. Nyinginezo kama hiyo zinazobeba kanuni ya utu kwa mujibu wa Omusikoyo (2021) ni *aliyekupa kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi, aliye juu mngoje chini, dunia ni kigeugeu, leo kwako kesho kwa mwenzako, kila kiwakacho huzima, kushuka ni mteremko kuliko kupanda, makuu hupwa, mali ni kama umande* na kadhalika.

***Uunganishwaji na Utegemeanaji***

Uunganishwaji na utegemeanaji ni miongoni mwa kanuni za ubuntu zilizofumbatwa katika methali za Kiswahili. Falsafa ya ubuntu inasisitiza uunganishwaji na utegemeanaji wa watu katika jamii. Inahoji kuwa watu wote katika jamii wameunganika na kuunda jamii pana. Huu uunganishwaji huashiria utegemeanaji na uwajibikaji wa pamoja kwa ustawi wa jamii. Ubuntu inasisitiza kuwa mtu ameunganishwa kwa mtu mwingine na utambulisho na utu wake kujengwa kupitia kwa mahusiano yake na watu wengine, (Eze, 2010). Kanuni hii imejitokeza katika methali nyingi za Kiswahili. Matumizi yake katika methali yanakuza umoja na ushirikiano wa jamii. Watu hukumbushwa kuwa hawawezi kufanikiwa peke yao ila kwa ushirikiano na watu wengine. Hivyo watu wasiopenda ushirikiano katika jamii hukumbushwa kwamba *mtu ni watu, kidole kimoja hakivunji chawa, umoja ni mshikamano, upweke ni uvundo, jifya moja haliinjiki chungu, haba na haba hujaza kibaba* na kadhalika. Methali hizi, zinafumbata maadili ya ushirikiano, utegemeanaji na uunganishwaji ambazo ni kanuni za ubuntu. Maadili hayo pia yanahimiza uwajibikiaji wengine ambao unawezekana tu kwa kuunganika na kutegemeana kwa watu. Venter (2004) anaeleza kuwa jamii inayotegemeana ni ile ambapo watu binafsi huweza tu kujitambua kupitia kwa wengine, huku wakitambua utofauti wa kibinafsi wa kila mtu. Breed na Semenya (2015) wanasema utegemeanaji unamaanisha pia kwamba binadamu hufungika na kushikanishwa pamoja kwa namna isiyoweza kutenganishwa. Hivyo jamii ikivunjika, mtu binafsi huvunjika. Inakuwa kwamba, urejesho wa jamii hauwezi kufanyika bila uponyaji wa mtu binafsi. Venter (2004) anahoji katika ubuntu kila mtu hujenga kiungo katika mnyororo wenye nguvu. Hivyo basi mtu hawezi kutimiza mengi pasipo kushirikiana na watu wengine.

***Heshima ya Binadamu***

Heshima kulingana na Kamusi ya Karne ya 21 (2019) ni tabia njema; adabu, thamani ya ubinadamu, utukufu, kitu ambacho mtu hupewa ikiwa ni ishara ya kuthaminiwa. Kanuni ya heshima ndani ya falsafa ya ubuntu inapania kutambua heshima na utu wa kila mtu na kukuza hisia za kuwa mmojawapo wa jamii na kuunganishwa. Ramose (1999) anahoji kuwa maadili ya heshima ndani ya falsafa ya ubuntu ni wajibu wa kimaadili. Ramose anaendelea kueleza kuwa ni wajibu wa kila mtu kuheshimu utu ulio ndani ya watu ili kuchangia katika ustawi wa pamoja wa jamii. Licha ya tofauti za usuli wa mtu, hadhi au imani, kila mtu ana haki ya kuheshimiwa na kushughulikiwa.

Methali zinazorejelea heshima huhimiza watu kuheshimiana kwa mfano methali *heshima kitu cha bure* kulingana na Wamitila (2001). Wamitila anaeleza heshima haigharimu chochote. Sio vigumu mtu kuwaheshimu wenzake. Wamitila (2001) anaeleza kuwa methali hii huhimiza watu kuheshimiana. Ulinzi wa heshima ya binadamu huhakikisha kuwa hakuna anayedharauliwa au kutendewa matendo yanayoshusha heshima yake (Chaskalson, 2002). Falsafa ya ubuntu inatambua

kuwa ni vigumu kujenga jamii imara yenye amani bila kuheshimu na kulinda heshima ya kila mwanajamii (Murithi, 2007). Heshima ya binadamu ni suala la kisheria ulimwenguni.

Suala la heshima ya binadamu lina nafasi katika Azimio Bia la Haki ya Binadamu na mataifa yote ulimwenguni yana kipengele cha sheria kinachohusu heshima ya binadamu katika katiba zao. Neal (2014) anahoji suala la heshima ya binadamu linatawala mifumo yote ya katiba za mataifa mbalimbali ulimwenguni, mawazo ya kisheria na nyanja mbalimbali za kiakademia. Kanuni ya falsafa ya ubuntu ya heshima ya binadamu inajitokeza pia katika simulizi za Waafrika zikiwemo methali kama vile *kila mtu ana heshima yake, kukosa heshima ni kama kufa, heshima ya mtu ni kama kioo, unapoivunja ni vigumu kuirekebisha, kuheshimu wengine ni kujiheshimu, ukizingatia adabu basi dunia yako itakuwa shwari, heshima si utumwa* na kadhalika. Methali hizo zinahimiza watu kuheshimiana ili kufanikisha uendeshaji wa jamii katika kila sekta. Kuwepo kwa methali nyingi zinazolenga maadili ya heshima ni thibitisho la upungufu wake katika jamii. Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa diskosi ya Fairclough (1992) ikitumikizwa kwa kanuni ya ubuntu ya heshima, watafiti wanaweza kufichua utata wa jinsi inavyotekelezwa, kueleweka na kutumikizwa katika miktadha tofauti pamoja na vile mabadiliko ya kijamii na kisiasa yanavyobainika katika jamii.

***Fadhila na Uelewa***

Ubuntu katika mawanda ya roho, hukuza heshima, msamaha na huruma kwa wengine (Rampa & Mphahlele, 2016). Katika ubuntu, binadamu huchukuliwa kuwa kiumbe cha kiroho kinachoongozwa na moyo pamoja na roho na sio kwa umantiki na fikra razini (Mamman & Zakaria, 2016). Mkabala huu kuhusu maadili unatofautiana na nadharia za kimaadili za Kimagharibi zinazosisitiza urazini na umantiki kama msingi wa maadili mema. Kanuni ya ubuntu ya fadhila na uelewa imekitwa pia katika methali za Kiswahili. Inakuza utamaduni wa fadhila kwa wengine. Inahimiza watu kuelewa na kuonyesha fadhila kwa tajriba, changamoto na mahitaji ya binadamu wenzao. Fadhila kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21 (2019) ni jambo jema ambalo mtu humfanyia mtu mwingine; hisani, ukarimu na wema. Gathogo (2008) anasema ingawa kuna uanuwai wa tamaduni ulimwenguni, falsafa ya ubuntu imesalia kama dira inayoelekeza mielekeo na tabia na kutoa faraja kwa watu wanaohitaji usaidizi.

Kulingana na falsafa ya ubuntu, mtu hahitaji kuwa anamjua mwingine kabla ya kumwonyesha fadhila, ubinadamu wao unatosha kustahiki kuonyeshwa fadhila. Kanuni ya fadhila na uelewa ya falsafa ya ubuntu imekitwa katika methali za Kiswahili. Kanuni hii inahimiza wanajamii kuonyeshana fadhila sawa na methali za Kiswahili ambamo kanuni hizi zimekitwa. Kulingana na methali hizo anayemtenda mwenzake wema, naye mema humwandama pia. Baadhi ya methali hizo ni *mwenye ihsani kutenda jamala naye hulipwa jamala, kila kitendo chema sadaka, kwendako mema hurudi mema, mtenda mema kwa watu atendea nafsiye, mtu awafanyaye watu mema naye Mungu humlipa mambo mema, fadhila ukitenda singoje kulipwa.* Methali hizi zinawahimiza wanajamii kutendeana mema ili kudumisha mshikamano na ustawi wa jamii.

***Mshikamano wa Jamii***

Hii kanuni ya ubuntu husisitiza umuhimu wa mshikamano wa jamii katika kuendeleza ustawi wa pamoja. Watu wanahimizwa kusaidiana na kuinuana kwa kutumia vitu kwa pamoja kwa maslahi ya jamii kwa jumla. Mshikamano ni hali ya kuwa na msimamo na ushirikiano katika kutimiza lengo fulani, Kamusi ya Karne ya 21 (2019). Jamii za Kiafrika zilihimiza mshikamano na ujamii. Maadili hayo yalikitwa katika methali, ngano na simulizi nyinginezo za Waafrika. Methali ya Kiswahili *umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.* Watu wakiungana kufanya jambo, matokeo huwa ya ufanisi, kwa upande ule mwingine, palipo na utengano, udhaifu hudhihirika. Kulingana na Fairclough (1992), diskosi za jamii na wajibu wa pamoja hukitwa katika shughuli za kijamii. Fairclough anahoji diskosi hizi zinapatikana katika hotuba, matini na njia nyinginezo za mawasiliano ambazo methali ni mojawapo. Hivyo basi methali za Kiswahili zinaakisi na kuzalisha kanuni za ubuntu kama dira ya maadili ya Waafrika.

Baadhi ya methali nyinginezo za Kiswahili zenye maana sawia na hiyo ni *gunia tupu halisimami wima, dau la upweke haliendi joshi, mafiga mawili hayaivishi chungu, jito likinenepa ni sababu ya mito mingine, kamba haipandi bila mti, mtu ni watu* na kadhalika. Methali zilizokitwa kanuni hii ya ubuntu hukuza dhana ya 'Nipo kwa sababu tupo" kama wanavyosema Mamman na Zakaria (2016).

Methali hizi zinakumbusha wanajamii kuwa hawawezi kuishi bila kushikamana na wengine katika jamii. Ujamii na mshikamano huwa kama gundi inayowaleta pamoja na kupinga changamoto zinazowakabili kwa jitihada za pamoja. Mshikamano wa kijamii hutoa ustawi wa kihisia kwa watu binafsi wanajamii wanapohisi kuwa wana wajibu wa kimaadili wa kusaidia wenzao wanapokuwa na mfadhaiko wa kihisia. Maadili hayo ya kuwajibikia wengine katika jamii yamekitwa katika methali za Kiswahili na hupigiwa watu wasiopenda kushirikiana na wengine katika jamii. Falsafa ya ubuntu inasisitiza wajibu wa pamoja wa jamii na wajibu ambao watu binafsi wanatekeleza kwa ustawi wa jamii nzima.

***Dhana ya Haki ya Mazingira***

Dhana ya haki ya mazingira imefumbatwa katika falsafa ya ubuntu. Mazingira yamekuwa sehemu mojawapo ya binadamu. Uhusiano baina ya mazingira na binadamu ni wa kutegemeana na kukamilishana. Kabla ya majilio ya wakoloni, Waafrika hawakuwa na dhana ya umiliki wa mashamba wala hatimiliki za mashamba (Asante, 2003). Katika jamii za kitamaduni za Kiafrika, wanajamii walikuwa na wajibu wa kutunza ardhi ya jamii, maji, misitu na mali asili nyinginezo. Kila mtu alitarajiwa kuacha mahali katika hali nzuri zaidi kuliko alivyopapata. Huenda methali zilifumbata ujumbe uliohusiana na masuala ya mazingira ili kuhamasisha wanajamii kuyatunza kwa ajili ya ustawi wao. Kuna methali za Kiswahili zinazohimiza maadili hayo kwa mfano *mchama ago hanyeli huenda akauya papo, daraja lililokuvusha usilitukane, livushalo ni gogo, pango ulimojisetiri usilidharau, ukipata chungu kipya usitupe cha zamani, unapopanda ukafika juu usitupe ngazi, usinyie kambi, huenda ukauya papo, usitukane ukunga uzazi ungaliko, usile kwa sahani ukasahau bunguu* na kadhalika. Thamani ambayo Waafrika waliweka juu ya mazingira yao inajitokeza katika simulizi zao zikiwemo methali za Kiswahili.

Maitaria na Mwita (2021) wanabainisha mazingira jinsi yalivyojitokeza katika methali za Kiswahili. Wanazuoni hawa wanaonyesha methali zinazorejelea miti kwa mfano *penye miti hakuna wajenzi* ambapo hali hiyo inaonyesha kuwa ni shughuli za binadamu zinazochangia uharibifu wa mazingira. Baadhi ya methali ambamo mazingira yanaakisiwa katika makala yao ni *mama msufi, baba msonobari, masukuzi ya leo ni msitu wa kesho, uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti, mali ni kama maua, mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi, maji hayakawii ila mtoni, maisha ni mlima, mawimbi ya habari mfalme, alisifuye jua limemwangaza* na kadhalika. Hivyo basi methali za Kiswahili kama vile falsafa ya ubuntu zinahimiza malezi ya mazingira kwa ajili ya ustawi wa jamii. Mara nyingi methali huakisi mazingira ya jamii zinamobuniwa, hali hii inathibitisha kuwa Waafrika waliyathamini mazingira yao na kuyaona kama kitovu cha uhai wao.

**Hitimisho**

Imebainika dhahiri kuwa kanuni za falsafa ya ubuntu kama dira ya maadili zimekitwa katika methali za Kiswahili. Kabla ya majilio ya wakoloni, Waafrika walitegemea simulizi zao kuadilisha na kuelimisha jamii. Hivyo basi methali za Kiswahili zikawa mojawapo ya nyenzo zilizopitisha maadili hayo kutoka kizazi hadi kingine. Kanuni za ubuntu kama vile fadhila, mshikamano wa jamii, umoja, utu, heshima ya binadamu, upendo na malezi ya mazingira zote zimefumbatwa katika methali za Kiswahili. Neno ubuntu lilitokana na methali ya Kinguni, hii ina maana kuwa simulizi za Waafrika ndizo ziliongoza namna walivyoishi. Hivyo hakuna mpaka baina ya kanuni za falsafa ya ubuntu na maadili yaliyomo katika methali za Kiswahili na methali nyinginezo za jamii za Waafrika. Kanuni za ubuntu zingali zinazingatiwa katika Afrika licha ya kwamba kuna athari nyingi za kigeni zinazotishia kuziangamiza. Hata hivyo ubuntu unaonekana kumezwa na falsafa za Kimagharibi za ubinafsi. Kizazi cha sasa kinauona kama ukale, mtazamo huu ndio mmojawapo wa mambo ambayo yamechangia uozo wa kimaadili katika jamii za hivi sasa barani Afrika.

**Marejeleo**

Akaka, L. na Wandera-Simwa. (2024). Iktibasi katika Methali za Waswahili. *Kiswahili*, *86*(2).

Asante, M. K. (2003). *Afrocentricity: The Theory of Social Change*. Chicago: African American Images.

Binsbergen, W. V. (2001). Ubuntu and the Globalisation of Southern African Thought and Society, *1*(2), 53-89.

Breed, G. na Semenya, K. (2015). *Ubuntu, Koinonia and Diakonia, a Way to Reconciliation in South Africa? 71*(2), 1-9.

Chaskalson, A. (2002). Human Dignity as a Constitutional Value of our Constitutional Order. *South African Journal on Human Rights*, *16*, 193-205.

Cilliers, J. (2008). *In Search of Meaning between Ubuntu and into: Perspectives on Preaching in Post-Apartheid South Africa*. A Paper Presented at the Eighth International Conference of Societas (Societas Homiletica), Copenhagen.

Eze, M. O. (2010). *Intellectual History in Contemporary South Africa*. Palgrave Macmillan.

Gade, C. B. N. (2011). The Historical Development of the Written Discourses on Ubuntu. *South African Journal of Philosophy, 30*(3).

Gathogo, J. (2008). African Philosophy as Expressed in the Concepts of Hospitality and Ubuntu. *Journal of Theology for Southern Africa*, *130*, 39.

Hailey, J. (2008). *Ubuntu: A Literature Review*. London: Tutu Foundation.

Kamusi ya Karne ya 21. (2019). Nairobi: Longhorn Publishers.

Kitula, K. na Ndalu, A. (1989). *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* EAEP.

Komparic, A. (2015). The Ethics of Introducing GMOs into Sub-Saharan Africa: Considerations from the Sub-Saharan African Theory of Ubuntu. *Bioethics 29*(9), 604-612. https://doi.org/10.1111/bioe.12191

Kress, G. (2010). *Multimodality: A Social Semiotic Approach to Contemporary Communication*. Routledge.

Maitaria, J. N. (2021). Methali za Kiswahili katika Ubainishaji na Uhifadhi wa Mazingira. *Taaluma, Jarida la Chakita*, *1*(1), 73-81.

Mamman, A., & Zakaria, H. B. (2016). Spirituality and Ubuntu as the Foundation for Building African Institutions, Organizations and Leaders. *Journal of Management, Spirituality & Religion*, *13*(3), 246-265.

Mayaka, B., & Truell, R. (2021). Ubuntu and its Potential Impact on the International Social Work Profession. *International Social Work*, *64*(5), 649-662.

Mbendera, R. (2020). Ubuntu Ethical and Values and Africa's Quest For a Better Home. *American Journal of Humanities and Social Sciences Research (AJHSSR*), *4*(8), 177-187.

Metz, T. (2007). Ubuntu as a Moral Theory: Reply to Four Critics. *S Afr J Philos., 26*(4), 369- 387. http://doi.org/10.4314/sajpem.v26i4.31495

Metz, T. (2009). The Final Ends of Higher Education in Light of an African Moral Theory. *J Philos Edu., 43*(2), 179-201. https://doi.org/10.1111/j.1467-9752.2009.00689.x

Metz, T. (2017). A Bioethic of Communion: Beyond Care and the Four Principles with Regard to Reproduction. In Soniewicka M., (Ed.), *The Ethics of Reproductive Genetics – Between Utility, Principles and Virtues*. New York, NY: Springer International Publishing AG,

Mugumbate, J., & Chereni, A. (2019). Using African Ubuntu Theory in Social Work with Children in Zimbabwe. *African Journal of Social Work, 9*.

Murithi, T. (2007). A Local Response to the Global Human Rights Standards: The Ubuntu Perspective on Human Dignity. *Globalisation, Societies and Education, 5*(3), 277-286.

Neal, M. (2014). Respect for Human Dignity as 'Substantive Basic Norm.' *International Journal of Law in Context*, *10*(1), 26-46.

Nyaumwe, L. J., & Mkabela. (2007). Revisiting the Traditional African Cultural Framework of Ubuntuism: A Theoretical Perspective. 6:152-163.

Ramose, M. B. (1999). *African Philosophy Through Ubuntu*. Mond Books

Rampa, S. H., & Mphahlele, L. K. (2016). Supporting Open Distance Learning (ODL) Students through Ubuntu Values. *Open Distance Learning (ODL) through the Philosophy of Ubuntu*, 119-132.

Sumba, O. T. (2021). Dira ya Methali. African Ink Publishers (Kenya).

Van Dijk, T. A. (2008). *Discourse and Context: A Sociocognitive Approach*. Cambridge University Press.

Van Leeuwen, T. (2008). *Discourse and Practice: New Tools for Critical Discourse Analysis*. Oxford University Press.

Venter, E. (2004). The Notion of Ubuntu and Communalism in African Educational Discourse. *Stud Philos Educ, 23*(2/3), 149-160.

Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

West, A. (2013). Ubuntu and Business Ethics: Problems, Perspectives and Prospects. *J Bus Ethics 121*(1), 1-https://doi.org/10.1007/s10551-013-1669-3

Wodak, R. (1989). *Language, Power, and Ideology: Studies in Political Discourse*. John Benjamins Publishing Company.

Wood, A. W. (2008). *Kantian Ethics*. Cambridge University Press.